KAZI
ZENYE MUSKTAKABALI MZURI ZAIDI
VERMONT



2027-2028
TOLEO LA





KAZI
ZINAZOWEZA KUKUPA MAPATO ZAIDI ZA
VERMONT

Kila kazi iliyoorodheshwa hapa inakadiriwa kulipa mshahara wa wastani wa zaidi ya $32 kwa saa na kuwa na angalau nafasi 300 katika jimbo kati ya 2024-2034.

Unajiuliza uanzie wapi?

Zingatia kazi iliyoandikwa kwa herufi nzito katika kila jedwali, ambazo zinatarajiwa kuwa na idadi kubwa zaidi ya nafasi za kazi.

Kumbuka kuwa:

- Mishahara ni fedha zinazolipwa moja kwa moja kwa wafanyakazi.
- Mshahara wa wastani ndio kiwango cha katikati kwa kazi hii: nusu ya watu hupata mshahara zaidi, na nusu hupata mshahara ulio chini ya kiwango hicho.
- Kumbuka kuwa mishahara inategemea uzoefu, elimu, na ujuzi.
- Ikiwa ni mara yako ya kwanza kufanya kazi fulani au una elimu ya chini, mshahara wa kuanzia unaweza kuwa mdogo.
- Waajiri wanaweza pia kutoa marupurupu pamoja na mishahara.

Je, ungependa kujua kuhusu kazi ambayo haijaorodheshwa hapa?

Kuna kazi nyingine nyingi nzuri zinazopatikana katika jimbo la Vermont – kama vile wafanyakazi wa posta, watunzaji wa kumbukumbu za fedha, makanika wa injini za dizeli, wasanifu majengo na madaktari wa mifugo.

Kwa usaidizi wa bila malipo wa kuandaa wasifu kazi, kupata maelezo zaidi kuhusu fursa za mafunzo, na kuunganishwa na mshauri wa masuala ya ajira, tembelea Vermont Department of Labor Job Center (Kituo cha Ajira cha Idara ya Kazi ya Vermont) katika eneo lako. Ili kupata maelezo zaidi kuhusu kazi hizi zinazoweza kukupa mapato zaidi na njia za kuzipata, tembelea: **mcclurevt.org/jobs**

ambapo utapata nyenzo kama: MyFutureVT.org



Vince

Mwalimu wa Darasa la 5 | Hardwick Elementary

- Shahada ya Kwanza
- Mpango wa Uanagenzi kwa Walimu wa Vermont
- Leseni ya Ualimu

SEHEMU NINAYOPENDA ZAIDI YA KAZI YANGU:

“Walimu wana athari kubwa sana kwa jamii, zaidi ya nilivyowahi kufikiria kabla ya kubadili taaluma.”



Margot

Mwanasayansi wa Mazingira | Jimbo la Vermont

Shahada ya Kwanza
Cheti cha Mhandisi Anayepokea Mafunzo
Leseni ya Mhandisi Mtaalamu

SEHEMU NINAYOIPENDA ZAIDI KATIKA KAZI HII:

"Kujionea miundombinu ya Vermont kwa karibu na kufurahia uzuri wa jimbo hili kupitia mtazamo wa usalama wa mabwawa ni mambo ambayo nisingeyaona kama si kazi yangu."

Je, wewe ni **mtu anayependa mpangilio na unazingatia kwa makini maelezo yote** na unapenda **kufanya kazi kwenye mazingira yenye maelezo mengi**?

KAZI ZINAZOWEZA KUKUPA MAPATO ZAIDI	Nafasi za Kazi Zinazotarajiwa Katika Miaka 10	Kiwango cha Chini cha Elimu Kinachohitajika Ili Kujiunga	Mshahara wa Wastani (kwa saa/kwa mwaka)
Maafisa wa Polisi	820	Shule ya Upili + Mafunzo	$35/$73,819
Wasaidizi Watendaji wa Usimamizi	780	Shule ya Upili + Mafunzo	$36/$75,802
Wasaidizi wa Kisheria	750	Shahada ya ngazi ya kati	$35/$71,947
Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu	**2,280**	Shahada ya kwanza	$41/$84,514
Maafisa wa Uzingatiaji	1,530	Shahada ya kwanza	$47/$96,858
Wachambuzi wa Usimamizi	1,310	Shahada ya kwanza	$55/$115,173
Wachambuzi wa Utafiti wa Soko	950	Shahada ya kwanza	$39/$80,213
Mawakala wa Wanunuzi na Ununuzi	840	Shahada ya kwanza	$34/$69,986
Wataalamu wa Usimamizi wa Miradi	550	Shahada ya kwanza	$42/$86,564
Wathamini na Wakadiriaji wa Mali	400	Shahada ya kwanza	$35/$72,794
Wakadiriaji wa Gharama	350	Shahada ya kwanza	$42/$87,187
Wachambuzi wa Mifumo ya Kompyuta	340	Shahada ya kwanza	$51/$106,706
Mawakili	560	Shahada ya uzamivu	$66/$136,385

Je, unapenda **kuchunguza, kufahamu, kuchambua, na kutatua matatizo**?

KAZI ZINAZOWEZA KUKUPA MAPATO ZAIDI	Nafasi za Kazi Zinazotarajiwa Katika Miaka 10	Kiwango cha Chini cha Elimu Kinachohitajika Ili Kujiunga	Mshahara wa Wastani (kwa saa/kwa mwaka)
Wauguzi Walio na Leseni	1,150	Mpango wa Mafunzo ya Cheti	$36/$74,910
Wataalamu wa Usaidizi wa Kompyuta	1,060	Mpango wa Mafunzo ya Cheti	$32/$67,513
Wauguzi Waliosajiliwa	**4,050**	Shahada ya kwanza	$50/$104,411
Watengenezaji Programu	1,220	Shahada ya kwanza	$65/$134,201
Wanasayansi wa Mazingira	410	Shahada ya kwanza	$40/$82,976
Wataalamu wa Maabara za Tiba	300	Shahada ya kwanza	$41/$84,291
Wauguzi Wataalamu wa Huduma za Afya	590	Shahada ya uzamili	$69/$144,339
Wanapatholojia wa Matamshi na Lugha	300	Shahada ya uzamili	$42/$87,945
Wasaidizi wa Madaktari	300	Shahada ya uzamili	$78/$161,207
Wataalamu wa Tiba ya Mwili	360	Shahada ya uzamivu	$50/$104,946

Mafunzo ya uanagenzi, vyeti, leseni na shahada huonyesha kuwa una ujuzi wa kazi fulani.



Collin

Mtaalamu wa Usaidizi wa Kompyuta | Champlain College

Cheti cha Usalama wa Mtandaoni
Shahada ya Ngazi ya Kati

Je, unapenda **kufanya kazi na watu** na **kutumia ubunifu wako** kuongoza au kushawishi?

KAZI ZINAZOWEZA KUKUPA MAPATO ZAIDI	Nafasi za Kazi Zinazotarajiwa Katika Miaka 10	Kiwango cha Chini cha Elimu Kinachohitajika Ili Kujiunga	Mshahara wa Wastani (kwa saa/kwa mwaka)
Wawakilishi wa Mauzo (Bidhaa na Huduma)	3,670	Shule ya Upili + Mafunzo	$41/$85,370
Mawakala wa Mauzo ya Bima	880	Shule ya Upili + Mafunzo	$36/$75,757
Walimu, Chekechea hadi darasa la 12 (ikijumuisha elimu Maalum na CTE (Elimu ya Taaluma na Ufundi))	**6,010**	Shahada ya kwanza	na/$75,907
Wataalamu wa Rasilimali Watu	1,140	Shahada ya kwanza	$40/$83,333
Wataalamu wa Mahusiano ya Umma	1,000	Shahada ya kwanza	$34/$70,766
Wahariri, Waandishi na Watunzi wa Vitabu	860	Shahada ya kwanza	$43/$90,186
Wahandisi wa Mauzo	800	Shahada ya kwanza	$60/$125,111
Wasanifu wa Picha	530	Shahada ya kwanza	$34/$70,365
Wataalamu wa Mafunzo na Ukuaji	500	Shahada ya kwanza	$40/$83,355
Wafanyakazi wa Kijamii wa Watoto, Familia na Shule	490	Shahada ya kwanza	$35/$72,147
Washauri Binafsi wa Kifedha	410	Shahada ya kwanza	$57/$117,847
Wapangaji wa Hafla	410	Shahada ya kwanza	$38/$79,612
Wachangishaji Fedha	330	Shahada ya kwanza	$37/$77,696
Washauri wa Matumizi ya Dawa za Kulevya, Matatizo ya Tabia na Afya ya Akili	1,210	Shahada ya uzamili	$32/$66,221
Washauri wa Shule na Kazi	770	Shahada ya uzamili	$33/$69,162
Waratibu wa Mafundisho	720	Shahada ya uzamili	$40/$83,934
Wafanyakazi wa Kijamii wa Afya, Matumizi ya Dawa za Kulevya na Afya ya Akili	720	Shahada ya uzamili	$39/$82,121
Watunza Maktaba	540	Shahada ya uzamili	$32/$66,800

Tafuta mshale unaoonyesha jinsi sifa na vyeti vinavyoweza kuunganishwa ili kukuza taaluma yako.

Je, unapenda **kufanya kazi kwa mikono yako au kutumia mashine** kutengeneza, kurekebisha, au kujenga vitu?

KAZI ZINAZOWEZA KUKUPA MAPATO ZAIDI	Nafasi za Kazi Zinazotarajiwa Katika Miaka 10	Kiwango cha Chini cha Elimu Kinachohitajika Ili Kujiunga	Mshahara wa Wastani (kwa saa/kwa mwaka)
Maseremala	**4,140**	Shule ya Upili + Mafunzo	$32/$66,844
Wapishi Mahiri na Wapishi Wakuu	840	Shule ya Upili + Mafunzo	$34/$70,098
Wakataji na Wapogaji wa Miti	770	Shule ya Upili + Mafunzo	$32/$66,599
Makanika wa Mitambo ya Viwandani	680	Shule ya Upili + Mafunzo	$33/$67,669
Waashi (Mawe, Matofali, Saruji)	420	Shule ya Upili + Mafunzo	$32/$65,703
Watengeneza Mashine	410	Shule ya Upili + Mafunzo	$32/$67,156
Walehemu Vyuma	370	Shule ya Upili + Mafunzo	$32/$65,520
Waendeshaji wa Mitambo ya Kusafisha Maji Taka	320	Shule ya Upili + Mafunzo	$33/$68,181
Fundi Umeme	1,600	Mpango wa Uanagenzi Uliosajiliwa	$33/$67,936
Fundi wa Mifumo ya Kupasha Joto, Viyoyozi na Jokofu	1,180	Mpango wa Uanagenzi Uliosajiliwa	$32/$66,577
Mafundi Bomba	990	Mpango wa Uanagenzi Uliosajiliwa	$32/$66,599
Wafanyakazi wa Ufungaji wa Nyaya za Umeme na Mawasiliano	420	Mpango wa Uanagenzi Uliosajiliwa	$44/$92,144
Mafundi wa Uhandisi (Ujenzi wa Miundombinu, Umeme, Viwanda)	510	Shahada ya ngazi ya kati	$38/$79,464
Wataalamu wa Usafishaji wa Meno	350	Shahada ya ngazi ya kati	$50/$104,411
Wahandisi (Uhandisi wa Ujenzi wa Miundombinu, Umeme, Viwanda, na Mitambo)	1,650	Shahada ya kwanza	$54/$111,876

Inaonyesha kuwa mtu anaweza kujifunza kazi hii kupitia mpango wa Mafunzo ya Uanagenzi Unaolipwa na Uliosajiliwa katika Jimbo la Vermont.



Sophia

Seremala |
Lewis Creek Builders
Vermont Works for Women
Mpango wa Mafunzo ya Kabla ya Uanagenzi kwa Vijana

VERMONT
DEPARTMENT OF LABOR

Idara ya Kazi ya Vermont (Vermont Department of Labor, VDOL) ipo ili kuboresha maisha ya wakazi wa Vermont wanaofanya kazi. Idara inatoa huduma kwa watu na biashara za jimbo ili wakazi wote wa Vermont waishi vizuri, wawe salama, na wapate ajira nzuri.

Nyenzo hii imetayarishwa kwa kutumia Makadirio ya Muda Mrefu ya Kazi ya VDOL yaliyotolewa mnamo Septemba 2026 yenye data ya mishahara ya 2025 hadi 2027.

THE J. WARREN & LOIS MCCLURE FOUNDATION

Shirika tanzu la Vermont Community Foundation lenye maono ya kuona jamii za Vermont zilizostawi, ambapo kila kijana anaweza kufanya mambo yanayomvutia na kujenga njia kuelekea kazi inayoweza kumpa mapato zaidi.

Kwa tafsiri za maelezo haya, kuomba brosha za bila malipo, na kupata nyenzo za kazi, tembelea

mcclurevt.org/jobs.

Utafiti: VDOL

Novemba 2026

Picha kwa Hisani ya: BETA Technologies | Community College of Vermont | HELM Construction Solutions | Jeb Wallace-Brodeur | Jeremy Baldwin | Lewis Creek Builders | New Frameworks | University of Vermont Health Network | Vermont Works for Women | Yestermorrow Design/Build School